**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# MAONI YA MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2017/2018

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**

Aprili, 2017.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA, MHESHIMIWA PAULINE PHILIPO GEKUL (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS –MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 NA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/18**

*Chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge,*

*Toleo la Januari, 2016*

## A. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake kwa kunipa uhai na afya ya kusimama hapa mbele ya Bunge lako tukufu siku ya leo, pia niwashukuru waheshimiwa wabunge na wananchi wote kwa sala na maombi yao nilipokuwa hospitalini baada ya kupata ajali nikiwa kwenye kazi zangu za kuwahudumia wananchi wa Jimbo langu la Babati Mjini. Nawashukuru sana tena sana!!!!

**Mheshimiwa Spika,** natoa shukurani zangu kwako wewe kunipa fursa ya kusimama hapa kuweza kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kuhusu utendaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa pekee naomba niishukuru familia yangu kwa uvumilivu mkubwa, na pia niwapongeze viongozi wote wa chama cha Demokrasia na Maendeleo wakiongozwa na Mwenyekiti wake ambaye pia ni KRUB kwa kumaliza salama ziara waliyoifanya kanda zote za kichama za nchi yetu na kuweka uongozi.

## B. MABADILIKO YA TABIANCHI

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabianchi ni mabadiliko ya mfumo wa hali ya hewa yanayosababishwa na kazi za moja kwa moja au zisizo za moja kwa moja za binadamu, ambazo zinaongeza gesi joto (Greenhouse Gases) na kubadilisha mchanganyiko wa viwango vya gesi katika angahewa la dunia, ambayo pia ni nyongeza ya mabadiliko ya asili ya mfumo wa hali ya hewa yaliyotathminiwa na kulinganishwa kwa muda mrefu (usiopungua miaka thelatini na zaidi).

**Mheshimiwa Spika**, aidha, Mabadiliko ya tabianchi kwa kiasi kikubwa (zaidi ya 95%) yanasababishwa na shughuli za kibinadamu ikiwemo uzalishaji wa viwanda unaotoa gesi ukaa (carbondioxide) kwa kiwango kikubwa sana.. Matokeo au athari za mabadiliko ya tabianchi ni; kuongezeka kwa joto, mvua kali/kubwa na za muda mfupi, mafuriko, mvua ya mawe ikiambatana na upepo mkali, mvua fupi zisizo za

msimu, na ukame wa muda mrefu na unaojirudia mara kwa mara. Haya mambo yote tayari yanajionesha hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabianchi, ambayo pia huchangiwa na uharibifu mkubwa wa mazingira umeleta athari kubwa katika sekta mbalimbali za maendeleo ya jamii na sekta zingine ziko katika hatari ya kuathirika pia, sekta hizi ni nishati, kilimo na usalama wa chakula, maji, mifugo (kwa kuzuka kwa magonjwa ya milipuko, ukosaji wa malisho na maji), uvuvi, misitu, wanyamapori, afya, miundombinu, utalii, n.k

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba mabadiliko ya Tabianchi sio nadharia za kwenye vitabu tu kama ambavyo watu wengi pamoja na Serikali inavyoamini, bali ni jambo la uhalisia usiokuwa na hata chembe ya mashaka kama ripoti mbalimbali za kisayansi zinavyothibitisha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mara ya kwanza katika uwepo wa Wilaya ya Karagwe ambayo ni moja ya wazalishaji wakuu wa zao la Kahawa na wazalishaji wakubwa wa ndizi, walikumbwa na ukame ambao ulikausha mibuni na migomba na ikalazimu kuomba msaada wa chakula, na pia ni wafugaji wakubwa wa ng'ombe aina ya Nyankole, lakini na mifugo yao ilikufa na wafugaji wengine iliwalazimu kuhamia maeneo mengine ya nchi ambayo yalikuwa

hayajaathirika na ukame ili kunusuru mifugo yao iliyobakia jambo ambalo linaweza kusababisha migogoro (ikiwemo kati wakulima na wafugaji). Kambi Rasmi ya Upinzani inatahadharisha kuwa hizo dalili zinaingia moja kwa moja kwenye kuporomoka kwa uchumi wetu, kama tutashindwa kuwekeza vyema katika kupambana na kuthibiti mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ikiwa moja ya nchi zinazoendelea inahitaji wananchi wetu kujengewa uwezo wa kustahimili athari za mabadiliko ya tabianchi na hiyo kuwa ni kipaumbele cha kwanza. Upunguzaji wa uzalishaji na ongezeko la gesi joto iwe ni kipaumbele cha pili. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kwa kuzingatia mambo haya mawili ni dhahiri madhara yanayojitokeza au yanayonyemelea sekta muhimu kwa uchumi wa nchi zitakuwa zimesalimika au madhara yatapungua kwa kiwango kikubwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi hii ya Makamu wa Rais inatambua uzito wa tatizo la mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa joto kali hadi kufikia nyuzi joto 36, sambamba na hayo kumekuwa na mvua kubwa na za muda mfupi zilizosababisha mafuriko katika maeneo mbalimbali nchini, kuyeyuka kwa theluji ya mlima Kilimanjaro, kupungua kwa vina vya maji katika mabwawa, mito, maziwa, kuingia kwa maji chumvi katika nchi kavu/mashamba na vyanzo vya

maji (kunakotokana na kuongezeka kwa kina cha bahari), kubadiliko kwa majira ya mwaka n.k

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ukweli kwamba mabadiliko ya tabinchi ambayo yamebadili majira ya mwaka kwa kuyacheleweshа au kuyawaisha, na madhara yanayotokea kutokana na mabadiliko hayo mara nyingi yanakuwa ni kuharibika kwa miundombinu na pia watu kupoteza maisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba; uwekezaji unaofanyika kwenye miundombinu kwa kiwango hichohicho kiwekezwe katika sekta za kuzuia na kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Mfano, ujenzi wa viwanja vya ndege, mvua ya siku moja au masaa kadhaa tu inaweza kuharibu uwekezaji uliofanyika kwa miaka kadhaa, au miundombinu ya barabara na madaraja vinaweza kuharibiwa kwa muda mfupi sana.

**Mheshimiwa Spika,** kiangazi kilichopilitiliza muda wake kikiwa na joto kali sana, kilivyoteketeza mifugo na wanyamapori na hivyo kusababisha umasikini mkubwa kwa familia za wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kwa watu ambao wanaishi karibu na mito miaka hiyo haikuwa na shida, lakini kwa sasa inaonesha kuwa wanaishi mabondeni. Hii ni kutokana na ukweli kwamba mito mingi imejaa michanga au udongo na kusababisha mito kupanuka/ kusambaa na pindi mvua kidogo ikinyesha basi

yanatokea mafuriko makubwa na kuathiri watu waliokuwa wanaishi hapo miaka yote. Mfano mzuri ni mto Msimbazi kwa miaka ijayo ule mto utapotea kabisa na maji yatakuwa yanapita kila pahala na hivyo kupelekea madhara makubwa. Mfano mwingine ni ziwa Babati ambalo mvua kidogo zikinyesha husababisha madhara makubwa.

**Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni,** tunatambua mchakato unaoondelea wa kupitia Sera ya Taifa ya Mazingira (1997) ikiwa na lengo kati ya mengine kujumuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

Tunapenda kusisitiza kuwa athari za mabadiliko ya tabianchi ni kubwa sana kiuchumi, kijamii na kiusalama na hivyo inahitajika kuandaa sera mahususi ili kuyapa uzito unaostahili Aidha tunataka kujua tumejipanga vipi kutekeleza kwa vitendo mikataba yote ya kimataifa ambayo tumeiridhia inayohusiana na mabadiliko ya Tabianchi.

C.**MIRADI YENYE HARUFU YA UFISADI** :

**Mheshimiwa Spika**, katika hotuba yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mwaka 2016/17 tuliongelea ufisadi kwenye miradi miwili;

a. mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya jiji la Dar es salaam.

b. mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi maeneo ya pwani (Bagamoyo, Pangani, Rufiji na Zanzibar.

**Hivyo basi, Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni,** iliomba Ofisi ya Makamu wa Rais imtake Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanyie ukaguzi maalum (**Special Audit**) wa miradi tajwa hapo awali ya kupambana na mabadiliko ya Tabianchi, pamoja na miradi mingine yote iliyosimamiwa na kitengo cha Mabadiliko ya tabianchi kilichopo chini ya Idara ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano. Tunaomba kufahamishwa mrejesho wa hiyo special audit, kama kweli utumbuaji wa majipu ni ukweli au unaangalia sura za wahusika tu.

**D. MAZINGIRA**

**Mheshimiwa Spika,** kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikisisitiza kuwa kila sekta ina muktadha wake wa uharibifu wa mazingira. Na kwa kila sekta inahitaji mbinu tofauti ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira kwenye sekta husika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kilimo, dhana ya mazingira inajikita zaidi kwenye uharibifu wa udongo ***(Soil degradation)***, au kupungua kwa rutuba ya udongo na hivyo kupelekea mimea kushindwa kustawi vyema. Uharibifu wa

udongo kwa kiasi kikubwa unasababishwa na shughuli za kiuchumi za kila siku zinazofanyika, ziwe za kilimo, uchimbaji wa madini na mafuta, utumiaji uliopitiliza wa mbolea na viatilifu vyenye kemikali, ufugaji uliopitiliza katika eneo moja. Hizi shughuli zinazosababisha uharibifu wa udongo zimetungiwa sera, sheria na miongozo lakini bado hali ni mbaya.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani kurudia mambo ambayo yapo na yanaeleweka ni kama kupoteza muda wa Watanzania. Hoja ya msingi ni kwamba bila ya nia ya dhati ya utoaji wa fedha zinazohitajika kwa ukamilifu wake kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya mazingira, basi sera, sheria na miongozo inakuwa ni kazi bure.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo huo wa serikali kutokutoa fedha, programu nyingi za mazingira ya kuhifadhi misitu zimekwama kutekelezeka na hivyo athari nyingi za kimazingira yameanza kuonekana na nchi inaingia kwenye majanga ambayo yangeweza kuzuilika kama serikali ingechukulia kwa umakini unaotakiwa wa mipango na progamu za mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** ukiangalia randama ya Wizara kwenye Idara hii ya Mazingira, ni kwamba program na mipango karibia yote ya kuhifadhi mazingira inayosimamiwa na Baraza la Taifa la Uhifadhi na usimamizi wa mazingira pamoja na

uratibu wa utekelezaji wa mikataba ya kimataifa inayohusu mazingira. Zaid ya asilimia 80 ya fedha za utekelezaji kwa miradi na program husika zinategemewa kutoka nje ya nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema huu nao ni udhaifu kwani pale washirika wakishindwa kutimiza miadi tu au wakichelewa kutoa fedha, basi program na miradi inasimama.

**Mheshimiwa Spika**, tukumbuke kwamba watu wanaopata madhara kutokana na athari za kimazingira kwenye maeneo husika ni Watanzania, hivyo basi, ni jukumu la msingi kwa Tanzania kulinda na kuhakikisha usalama wa wananchi wake na usalama wa mazingira yanayowazunguka.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka kipaumbele kama inavyoweka kwenye sekta zingine katika kuhakikisha inatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha mipango inayopangwa kuhusiana na mazingira inatekelezwa kwa kadri ilivyopangwa. Sambamba na hilo ni kwamba katika miradi inayofadhiliiwa na taasisi na mashirika ya kimataifa kuna uwezekano mkubwa wa kuchepusha fedha au kutumika mbali ya kile kilichokusudiwa, hivyo ni muhimu sana miradi hiyo kuifanyia ukaguzi wa karibu na mara kwa mara. Mfano miradi ya kujengea watu uwezo ni rahisi sana fedha kutumika vibaya.

**Mheshimiwa Spika,** katika muktadha mzima wa uhifadhi wa mazingira, suala la maji ndiyo nguzo kuu. Hoja ya kwanza ni maji kiasi gani yanahitajika katika uhifadhi, maji hayo yanapatikana kutoka wapi, maji hayo yanakuwa katika aina ipi na je maji hayo yakishatumika kuna uwezekano wa maji hayo kutumika tena kwa kazi zile zile au kwa kazi tofauti? Na hoja nyingine ni je maji yakishatumika yanahifadhiwaje? Je kama ni maji ya mvua (run off) yanaingiaje kwenye mto na ni madhara gani yanatokea kwenye mto husika? Pia, utafiti katika kiwango na upatikanaji wa maji ardhini (underground water) bado hauridhishi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba hayo mambo tajwa ndiyo yanatoa uendelevu wa matumizi ya maji katika uhifadhi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, mazingira kwa muktadha wa uzalishaji na uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani "**e**missions, Effluent and Waste". Kuanzia hapo utunzaji wa mazingira ni kufahamu katika mchakato mzima wa uzalishaji viwandani ni wakati au eneo gani katika mchakato mzima wa uzalishaji unaozalisha kwa wingi gesi ukaa, ambayo inaleta madhara makubwa kwa watu na mazingira? Je kuna mbadala unaoweza kutumiwa katika hatua hiyo ya uzalishaji ili kukabiliana au kupunguza au kusitisha kabisa uzalishaji wa gesi ya ukaa katika mchakato huo wa uzalishaji bidhaa?

**Mheshimiwa Spika,** ni muhimu vile vile kufahamu ni wakati au hatua gani katika uzalishaji bidhaa unatoa taka "wastes" nyingi? Na taka hizo zinatunzwa au teketezwa vipi ili kuhifadhi mazingira? Na je kuna teknolojia mbadala ya kuzifanya taka hizo kutumika tena kwenye uzalishaji wa bidhaa hapo kiwandani au pahali pengine?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani, inafahamu kuwa kazi hizi ambazo zikifanywa na Wizara hii ya Mazingira, kwa kiasi kikubwa ili kuwa ni kutembelea viwandani na kukagua mifumo yao ya maji taka. Hoja ni kwamba viwanda vingi hapa nchini teknolojia yake ya uzalishaji imepitwa na wakati ambayo inapelekea uchafuzi wa mazingira. Hivyo viwanda kupigwa faini kutokana na kuzalisha kwa teknolojia iliyopitwa na wakati nakupelekea viwanda hivyo kufungwa na mwisho kulazimika kupunguza wafanyakazi na kutengeneza tatizo lingine la ukosefu wa ajira.

## E. MFUKO WA TAIFA WA DHAMANA YA HIFADHI YA MAZINGIRA

**Mheshimiwa Spika**, mfuko huu ulianzishwa kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa mazingira wa mwaka 2004 kama chanzo cha fedha kwa ajili ya kuhifadhi mazingira nchini. Lakini cha kushangaza hadi leo 2017 ndio Seriali inazindua mfuko huu pamoja na Sekretariat ya bodi ili kufanya kazi za mfuko. Hata hivyo katika bajeti ya mwaka hi shilingi milioni 334

zilizotengwa kwa ajili ya mfuko huu muhimu sana ambao ungesaidia kutatua changamoto za kimazingira fedha ambazo ni chache sana kukabiliana na masuala ya mazingira nchini.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kubainisha vyanzo vya mapato vya mfuko huu ili uwe endelevu na uwe na nguvu ya kifedha kuliko ilivyo sasa. Mfano wa vyanzo hivyo inaweza kuwa 10% ya kila makusanyo ya leseni za viwandani, madini, usafirishaji, utalii, tozo mbalimbali zinazotozwa na TFS. Na pia tozo ya 20% yajumla ya fedha zinazotozwa kwa bidhaa zinazoingizwa nchini na kutozwa ushuru wa uchakavu kwa ajli ya utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa fedha hizi ni dhahiri halmashauri zetu zitaweza kutekeleza miradi yote inayohusu utunzaji wa mazingira.

## F. BARAZA LA RUFAA LA MAZINGIRA

**Mheshimiwa Spika,** Baraza hili lipo kwa mujibu wa sheria ya mazingira ya mwaka 2004, kwa lengo la kusikiliza rufaa za wananchi ambao hawaridhiki na maamuzi ya Waziri na masuala mbalimbali katika utekelezaji wa sheria ya mazingira.

**Mheshimiwa Spika**,taarifa ya utekelezaji ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/17 inasema kuwa sasa hivi ndio Ofisi imeandaa hadidu za rejea za kutayarisha Mpango Mkakati wa Baraza la Rufaa la Mazingira ambao ukikamilika ndipo baraza litaanza kufanya kazi.

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba Waziri mwenye dhamana na Mazingira amekuwa akionekana mara nyingi akitembelea viwanda na kutoa adhabu ya fedha au na kusitisha uzalishaji wa viwanda husika. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata maeleze, Je, kama waathiriwa wa maamuzi ya waziri kama hawaridhiki, wanapataje haki zao wakati baraza la kupeleka malalamiko yao halipo?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani baada ya kupitia randama ya wizara imeshindwa kuona kifungu kinachoanzisha Baraza la Rufaa la Mazingira, hivyo tuna muomba Mheshimiwa Waziri Mwenye dhamana atuoneshe kifungu kinachotoa fedha za uanzishwaji na utendaji kazi wa Baraza.

## G.KAMPENI YA KITAIFA YA UPANDAJI MITI

**Mheshimiwa Spika,** kampeni ya kitaifa ya upandaji wa miti inaratibiwa na ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, lakini

halmashauri zetu zimepewa lengo la kupanda na kutunza miti isiyopungua milioni 1.5 kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa halmashauri zetu hazina fedha za kuzalishaji miche ya miti kwa idadi tajwa na pia haina uwezo wa kutunza miti hiyo kutokana na ukweli kwamba maeneo mengi hali ya maji sio nzuri.

**Mheshimiwa Spika**, kila eneo katika nchi yetu ina aina yake ya miti inayostawi kulingana na aina ya udongo kwenye maeneo husika, aidha, wilaya moja inaweza kuwa na aina tofauti za udongo kuweza kuhimili ustawi wa aina moja ya miti.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana alieleze Bunge, Ofisi yake inatoa kiasi gani au mchango gani wa kuzisaidia Halmashauri zetu ili ziweze kutekeleza zoezi la upandaji na utunzaji miti kwa ukamilifu wake? Tunauliza hivyo kutokana na ukweli kwamba Halmashauri zetu hazina vyanzo vya mapato vya kuweza kutekeleza agizo hilo la Ofisi ya Makamu wa Rais.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri wakala wa huduma za misitu (TFS) ipewe jukumu la kuzalisha miche

nchi nzima ambayo inalingana na aina ya udongo na hali ya hewa ya eneo husika. Aidha, kwa udhibiti wa fedha kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais itakuwa ni rahisi kuzifanyia udhibiti kuliko kupeleka fedha kwenye Halmashauri zetu. Hivyo basi, Shilingi bilioni 105 zinazohitajika katika utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya Upandaji wa Miti zitakuwa salama zaidi, bila ya kubadilishiwa matumizi yake.

## H. UZALISHAJI NA MATUMIZI YA MIFUKO YA PLASTIKI

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba Bunge la Afrika ya Mashariki lilipitisha Muswada "***The EAC Polythene Materials Control Bill, 2011***" ambao ulikuwa na lengo la kupiga marufuku uzalishaji, uuzaji, na uagizaji na matumizi vya "**polythene materials".** Na Serikali kupitia kwa Baraza la Usimamizi wa Mazingira likapiga marufuku hapa Tanzania ili kukazia sheria iliyotungwa na Bunge la Afrika ya Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, ni kweli vifungashio vya plastiki vinachafua mazingira na hilo halina mjadala, lakini mazingira kuwa machafu ni tatizo la uchafu wenyewe au ni tabia ya watu. Jambo hili linaweza kuwa jepesi kutamkwa lakini ni gumu kutekelezwa kutokana na ukweli kwamba uchafu huo vifungashio vya plastiki unaweza kuwa ni fursa kwa nchi yetu.

Kwa kuwa vifungashio hivyo vina **"recycle"** na kuweza kutoa bidhaa zingine, na kwa kuwa bidhaa nyingi zinazotoka nje ya nchi vinakuja vimefungwa kwa vifungashio vya plastiki, hii ni ishara kwamba nchi ambazo ni tajiri kutuzidi na hatuwezi kujilinganisha zao katika maendeleo ya kiuchumi bado wanazalisha na kutumia vifungashio vya plastiki.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona itakuwa ni busara mamlaka husika kuliangalia suala hili kwa upande wa kuwa fursa zaidi kuliko linavyoangaliwa.
Mfano mzuri sana ni kwa upande wa bidhaa hasa maziwa, lita moja iliyofungwa kwenye mifuko ya plastiki ni shilingi 500/- na kwa ujazo huo huo kwenye chupa yanauzwa kwa takriban shilingi 1500/-.  Tuangalie uhalisia wa wananchi wetu vijijini na aina gani ya vifungashio wanavovitumia zaidi. Baada ya kufanyia kazi jambo hilo ndio uamuzi stahiki unaweza tolewa.

## I. NISHATI MBADALA

**Mheshimiwa Spika**, kuna tatizo kubwa sana la nishati mbadala hapa nchini na hivyo kupelekea matumizi ya kuni na mkaa kuwa chanzo kikuu cha nishati inayotumiwa na zaidi ya watanzania asilimia 90. Jambo hili ni chanzo kikubwa cha ukame unaoyakumba maeneo mengi hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Nishati ya gesi kwa matumizi ya majumbani imekuwa ni tatizo kubwa sana kutokana na bei yake, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kama kweli Serikali ingekuwa imedhamiria suala hili la nishati ya gesi kuwa mbadala wa nishati ya kuni  kama inge unganisha nguvu za waagizaji wa nishati hiyo toka nje ili wajenge kiwanda cha kuchakata gesi inayozalishwa hapa kwetu na kuiweka kwenye mitungi na kuisambaza nchi nzima. Tunaamini kabisa kwamba bei yake itakuwa ni nafuu zaidi kuliko gesi inayoagizwa toka nje ya nchi.

## J. TAKATAKA KUZALISHA NISHATI MBADALA NA MBOLEA

**Mheshimiwa Spika,** Taka ngumu kawaida huitwa majina mengi-takataka, uchafu, masalia, mabaki na majina mengine, taka ngumu hazipaswi kusababisha matatizo ya kiafya. Zinaweza hata kuwa chanzo cha pato na rasilimali za kutengenezea bidhaa mpya. Lakini pale ambapo taka ngumu hazikusanywi ipasavyo, kutenganishwa, kutumika tena, kurejeshewa thamani au kuangamizwa kwa usalama, huweza kusababisha kichefuchefu, kutoa harufu mbaya, na kusababisha matatizo makubwa ya kiafya.

**Mheshimiwa Spika**, Taka ni changamoto karibu kila mahali kwa sababu tunaendelea kuzalisha taka nyingi sana. Na

kama tunavyoona kwenye maeneo yanayotuzunguka, taka kutokana na plastiki, glasi na chuma haziozi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuliona hilo Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni kwa ushirikiano na Jiji la Humburg Ujerumani walianzisha mradi wa kuchakata taka ili kuzalisha umeme na mbolea, lakini mradi huo hadi sasa bado haujaanza kutokana na mambo ambayo bado hayajakaa vizuri kwa upande wa ushuru wa kuingiza mitambo hiyo hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** jambo hilo ni jema kuwa mfano wa kuigwa kwa majiji na miji mingine hapa nchini, kwani ni chanzo cha ajira pamoja na uzalishaji wa mbolea. Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira inafahamu kuwa mradi huo wa kuchakata taka kwa Halmashauri ya Kinondoni umekwama wapi? Na inasaidia vipi katika kuhamasisha miradi mikubwa ya kuweka mazingira ya miji yetu kuwa safi?

## K. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA 2016/17 NA MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 2017/18

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira taarifa za utekelezaji hadi mwezi March, 2017 inaonesha kuwa kati ya kiasi cha shilingi bilioni 10.973 zilizopitishwa na Bunge ni asilimia 11.28 tu

sawa na shilingi bilioni 1.24. zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kati ya fedha hizo shilingi milioni 236.19 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1.001 ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, ukiangalia muhtasari wa bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/17 inaonesha kuwa fedha za ndani zilizopitishwa na bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 8 na hadi mwezi March, 2017 serikali imetoa shilingi milioni 236.17 ambazo ni sawa na asilimia 2.95 (2.95%). Hii maana yake ni kuonesha kuwa kukabiliana na athari za mazingira pamoja na mabadiliko ya tabianchi kwa ujumla wake sio kipaumbele cha Serikali yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kuna tatizo lingine katika taarifa za utekelezaji ambalo tunashindwa kufahamu kwamba kati ya fedha za ndani za miradi zilizopangwa, ni kiasi gani cha fedha kwa kila mradi zimetolewa hadi mwezi March, 2017. Kwani takwimu zinawekwa kwa ujumla tu, na hili linafanya tushindwe kuhoji kwa mradi fulani fedha zimetolewa au bado na kwa mwaka unaofuata kwa nini bajeti ipande au kushuka? Mfano Mradi ***Na. 5301- Climate change Adaptation Programme,*** fedha za ndani zilitengwa shilingi 3,200,000,000/- na fedha za nje, shilingi 2,594,633,448/-. Mradi huo huo kwa mwaka 2017/18 fedha za ndani umetengewa shilingi 850,000,000. Na fedha za nje shilingi 1,400,000,000/. Mradi Na. 5307 National Environmental Trust Fund mwaka unaomalizika

ulitengewa fedha za ndani shilingi 2,100,000,000/. Haieleweki ni kiasi gani kimetolewa na mwaka huu wa fedha mradi huo huo umetengewa jumla ya shilingi 334,454,000/.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza tena kuwa ni muhimu taarifa ya utekelezaji ikaonesha kwa kila mradi ni kiasi gani kimetolewa hadi mwezi March, 2017 wakati Wizara inapotayarisha taarifa hizo.

**Mheshimiwa Spika,**mpango wa maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/18 mchanganuo wa makadirio ya miradi ya maendeleo inaonesha kuwa kati ya fedha za ndani shilingi bilioni 3, shilingi bilioni 1 ni fedha ambazo matumizi yake hayaendani na usimamizi wa mazingira kama ambavyo ilikuwa katika mpango wa mwaka uliopita. Aidha kwa miradi inayosimamiwa na NEMC shilingi bilioni 2.056 ni kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** inaonesha kuwa mradi wa Kihansi Catchment Conservation Management Project wa gharama ya shilingi bilioni 2.057 unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Mheshimiwa Spika, haya maneno ya "ufadhili wa benki ya Dunia" kwa urahisi utadhani ni bure, lakini hakuna benki ambayo inatoa fedha za bure, ni lazima kuna masharti ya urejeshwaji wake. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona ingekuwa vyema kwa umuhimu wa sekta ya mazingira Serikali na taasisi zake ipange matumizi ya utekelezaji wa

miradi yake kwa kutumia fedha za ndani, kwani kutegemea ufadhili ni rahisi kutokea mkwamo ambao ungeweza kutatuliwa kama fedha zetu za ndani zingepangwa kwa shughuli hizo.

## L. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** "Mahatma Gandhi" baba wa Taifa la India aliwahi kusema kwamba ***"Earth provides enough to satisfy every man's need, but not every man's greed"***, kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba, "*dunia ina kila kitu cha kutimiza mahitaji ya mwanadamu, lakini sio kutimiza matamanio na ulafi wa binadamu*". Kwa muktadha huo ni kwamba, uchafuzi na uharibifu mkubwa wa mazingira katika Dunia hii, Tanzania ikiwa ni mojawapo ni tabia ya binadamu ya ulafi wa kutaka kumiliki kila kitu na katika mchakato wa kumiliki kila kitu ndipo uharibifu unapotokea.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mtazamo mwingine ni kwamba, kitendo cha kutompatia au kummilikisha binadamu kile kinachoweza kuendesha maisha yake na familia yake nalo ni tatizo, kwani kinachofanyika ni kutokutumia kiuendelevu raslimali zilizomzunguka.

Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa ushauri kwamba, ni muda mwafaka kwa Serikali kuwa na ile dhana kwamba maliasili ni mali ya umma, kwani kuwa mali ya umma hakuna mwenye

uchungu nayo katika suala zima la matumizi endelevu ya raslimali zetu.

**Mheshimiwa Spika,** ni muda mwafaka sasa kwa serikali kulipa kipaumbele suala la uendelevu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi katika utoaji wa fedha kama ambavyo sekta zingine za kiuchumi zinavyopewa kipaumbele katika upangaji na utoaji wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**Pauline Philipo Gekul (Mb)**

**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira.**

**24/04/2017**